

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

Julai/Agosti 2014

Muda: Saa 2½

**MTIHANI WA MAKADIRIO WA WILAYA YA GATUNDU**  
**CHETI CHA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI**

KISWAHILI

Karatasi ya

FASIHI

Muda: Saa 2 ½

**MAAGIZO**

- a) Jibu maswali MANNE pekee katika kijitabu cha majibu ulichopewa.
- b) Swalii la kwanza ni la LAZIMA.
- c) Chagua maswali mengine matatu kutoka sehemu zilizobakia yaani: Riwaya, Fasihi simulizi, shairi na Hadithi fupi.
- d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
- e) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigiwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

## SEHEMU A: TAMTHILIA

Timothy M. Arege: Mstahiki Meya.  
(Swali la Lazima)

1. "Wapo sana. Lakini tulipo ndio tuliochaguliwa.....kwa nini basi kulalamika?"
  - a) Eleza muktadha wa dondoo hili? (alama 4)
  - b) Fafanua kwa kutoa mifano sifa tatu za mzungumzaji? (alama 6)
  - c) Uusaliti na ukengeushi ni mionganoni mwa mambo muhimu yanayojitokeza katika tamthilia ya mstahiki meya. Thibitisha. (alama 10)

## SEHEMU B: RIWAYA

(Ibu swali la 2 au 3)  
Ken Walibora: Kidagaa kimewozea.

2. Kwa kutumia riwaya ya kidagaa kimemwozea jadili jinsi swala la ukoloni mamboleo na ultima limefanuliwa. (alama 20)
3. "alisimama dadidi na kuwatazama hawa watu wawili waliosimama wima kutetemeka kama waliokuwa wamepigwa na dhoruba ya theluji"
  - a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
  - b) Eleza hulka ya yule 'alisimama dadidi na kuwatazama hawa watu wawili.' (alama 6)
  - c) Jadili mchango wa wanawake katika riwaya ya kidagaa. (alama 10)

## SEHEMU C: USHAIRI

(Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata)

### RABI HUMLIPIZIA

Pungueni uonezi, wanyonge kuwaonea  
Kuwafanya wao mbuzi, mazizini kuwatia.  
Muogopeni Mwenyezi, haki mkiwapatia.  
Rabi humlipizia, Mnyonge mkosa haki.

Rabi kumeza hawezi, dhuluma isiyo njia,  
Atatoa uamuzi, haki inayopotea,  
Daima kwake machozi, kuna kilio kulia,  
Rabi humlipizia, Mnyonge mkosa haki.

Nyanenayo sadiki, alikilini kuyatia,  
Alosikilia haki, hatafikwa na hatia,  
Punguzeni unafiki, kuzua mkichelea  
Rabi humlipizia, Mnyonge mkosa haki.

Haki haifichamiki, japo iwe myaka mia  
Mwenyezi Mungu mwehaki, haki atafichua  
Awatenge wanafiki, haki mnaoumbua,  
Rabi humlipizia, Mnyonge mkosa haki.

Kuna kundi lake laki, limekaa langojea,  
Kukalia unafiki, mwashibota kuwania,  
Punguzeni mwabonaki, mumde mola jalia  
Rabi humlipizia, Mnyonge mkosa haki.

Rabi atawafedhehi, haki wanayoumbuwa,  
Na mwisho awakebehi, avunje wenu uluwa,  
Mwenzi wenu nimewahi, Mungu ameniokowa,  
Rabi humlipizia, Mnyonge mkosa haki.

(kutoka: Diwani ya Akilimali, Akilimali, S.E.AL.B; Uk 54)

### Maswali

- a) Taja umuhimu ya kutenda haki. (alama 4)
- b) Taja mbinu mbili za lugha zilizotumika katika shairi hili. (alama 2)
- c) Shairi hili linaweza kuwa katika bahari mbili. Zitaje (alama 2)
- d) Taja na ueleze mifano miwili tofauti ya uhuru wa kishairi uliotumika. (alama 2)
- e) Mshairi alikuwa na dhamira ipi alipotunga shairi ili. (alama 2)
- f) Andika ubeti wa 3 kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- g) Eleza muundo wa ubeti 2 (alama 2)
- h) Fafanua maana ya :
  - (i) Awatenge wanafiki, haki mnaoumbua.(alama 2)

### SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI

- 5. (i) Misimu ni nini (alama 2)
- (ii) Eleza sifa tano za misimu. (alama 10)
- (iii) Fafanua majukumu yoyote manne yanayotekelawa na misimu. (alama 8)

6. a) Maghani ni nini? (alama 2)

b) Eleza fani zifuatazo za maghani (alama 8)

- (i) Tondozi
- (ii) Pembezi
- (iii) Tendi
- (iv) Rara

c) Eleza sifa tata za maghani. (alama 6)

d) Taja dhina nne za maghani. (alama 4)

SEHEMU E: Hadhithi Fupi.

Ken walibora na Said A. Mohammed: Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.

7. Tukio lililowaleta hapa ni la kawaida kwetu. Ingawa sisi hufanya tuwezayo kuwalinda wanetu, mara nyingi tabia zao hutupiga chenga.....”

a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)

b) Eleza sifa nne za mzungumzaji. (alama 8)

c) Jadili matatizo manne yanayojitokeza katika hadithi hii. (alama 8)